

## Maswali

1. Mbona Waisraeli walitakiwa wawe na sheria mpya?
2. Nani aliwapa sheria za kutumia?
3. Mungu aliahidi nini ikiwa Waisraeli watampenda na kumtii
4. Watu walikubali kumpenda Mungu?
5. Siku ya tatu watu waliona na kusikia nini?
6. Amri gani ya kipekee yenye Mungu alipea watu?
7. Amri hizi ziliambia watu nini?
8. Mbona watu walitaka Mungu azungumze na Musa badala ya kuzunguza nao?
9. Mbona Musa alienda juu ya mlima?
10. Nini iliandikwa juu ya mawe mbili?

## Majibu

1. Waisraeli walitakiwa sheria ziwafundishe vile wanaweza kufurahisha Mungu na waishi vizuri pamoja.
2. Mungu aliwapa sheria.
3. Mungu aliahidi kuwalinda jangwani na kuwaongoza mpaka nchi aliyowaahidi.
4. Ndiyo, Watu waliahidi kutii Mungu.
5. Umeme, ngurumo, wingu mzito, moshi, tarumbeta ikichezwa na tetemeko ya nchi.
6. Amri kumi.
7. Vile watajiendeleza mbele ya Mungu, mbele ya wazazi wao, marafiki na majirani.
8. Watu waliogopa wakati Mungu aliwazungumzia.
9. Mungu alimwambia Musa aende juu ya mlima.
10. Amri kumi ziliandikwa kwa mawe mbili.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2 Mwaka wa 1



# 21 Amri kumi

**Kwa Biblia** Kutoka 19 na 20:1-21

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alipea Waisraeli amri za kuwaonyesha vile wanaweza kuishi. Tunalazimishwa kutii amri za Mungu kuonyesha tunampenda.

## Somo

Amri au sheria ni za maana sana. Sheria zinazaidia watu kuishi pamoja na amani tena kwa furaha. Kila jamii ina mashariti na sheria zao. Tuna sheria shuleni. Kila nchi ina sheria zake.

Waisraeli walikuwa watumwa Misri. Walipokuwa Misri walitii sheria za Misri. Sasa Waisraeli walikuwa huru kutoka Misri. Walikuwa taifa huru wakisafiri jangwani kuenda nchi waliyoahidiwa na Mungu. Waisraeli hawakukuwa na sheria zao. Waisraeli walihitaji sheria mpya za kuwasaidia waishi pamoja kwa furaha. Mungu alipea Waisraeli sheria zake kuwafanya wawe taifa kubwa.

Waisraeli walikuja kwa Mlima wa Sinai. Walipika kambi chini ya mlima. Mungu aliita Musa juu ya mlima. Mungu alimkumbusha Musa kwamba alikuwa amewaokoa kutoka Misri. Mungu alikuwa amewalinda safarini. Mungu alipenda Waisraeli. Aliwachagua kuwa watu wake wakipekee. Mungu alikuwa ameahadi Ibrahimu, Isaka na Israeli ahadi za kipekee. (Israeli alikuwa Yakobo mpaka Mungu alipompa jina la Israeli).

Ahadi za Mungu zilikuwa kwa Waisraeli waliokuwa wa uzao wa Israeli. Mungu alitaka Waisraeli wamtii na kumpenda. Kama Waisraeli watamtii Mungu, atawalinda na kuwafikisha salama kwa nchi aliyowaahidi

Musa aliteremka kutoka Mlima wa Sinai. Aliambia Waisraeli kila kitu chenye Mungu alisema. Waisraeli walifurahi kwa sababu Mungu alikuwa amewachagua kuwa taifa lake teule. Walifurahi kwamba Mungu atawalinda na awaongoze mpaka nchi aliyokuwa amewaahidi. Wote walisema, "Tutafanya yote yenye Mungu amesema."

Siku ya tatu kulikuwa na umeme na ngurumo. Mlima ulifunikwa na wingu nzito. Watu walisikia tarumbeta ikipigwa kwa sauti ya juu, na wote wakaogopa. Musa aliongoza watu kutoka kambini. Walisimama chini ya mlima. Moshi kama moto mingi ilitoka kwa mlima na kukawa na tetemeko kubwa ya nchi. Sauti ya tarumbeta iliendelea kuwa juu. Musa alizungumza na Mungu alimjibu. Mungu alishuka chini kwa Mlima wa Sinai na akapea Waisraeli Amri zake.

Mungu aliwapa Waisraeli amri kumi. Amri zingene ziliwambia vile wanaweza kujiendeleza mbele ya Mungu. Amri zingine zinawambia vile wanaweza kujiendeleza kwa wazazi wao, marafiki wao na majirani wao.

#### **Amri kumi**

Usiwe na miungu mingine ila mimi.  
Usichifanyie sanamu ya kuchonga.  
Usilitaje bure Jina la Mungu.  
Ikumbuke siku ya Sabato na uitakase  
Waheshimu baba yako na mama yako.  
Usiue  
Usizini  
Usiibe  
Usishuhudie uongo (kusema uongo)  
Usitamani (kutaka vitu visivyo vyako)

Watu waliogopa sana. Waliogopa wakati Mungu alizungumza nao. Waliogopa moto, tarumbeta na mtetemeko wa nchi. Watu waliuliza kama Mungu angezungumza na Musa. Hawakutaka Mungu azungumze nao. Walitaka Musa azungumze na Mungu halafu awambie vile Mungu amesema.

Mungu alimwambia Musa aende juu ya mlima. Huko Mungu alizungumza na Musa. Mungu alimpa Musa sheria zenye Waisraeli wanapaswa kutumia. Mungu alimweelezea vile alitaka Waisraeli wamwabudu. Mungu aliandika amri kumi za kipekee kwa mawe mbili. Mungu akamwambia Musa aweke hizo mawe vizuri na awafundishe Waisraeli amri kumi.

